

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI



SAYEH AZITAKA NCHI ZA AFRIKA KUWA NA SERA MADHUBUTI

“Kushuka kwa uchumi katika nchi zilizoko katika jangwa la Sahara kunaweza kukawa si kuzuri sana. Pato linategemewa kuwa asilimia 4³/₄ mwaka 2010, ukilinganisha na asilimia 2 ya mwaka 2009. Pamoja na kuwa uchumi wa Dunia unaendelea na kukua, uchumi katika eneo letu ungepaswa kuendelea lakini mpaka kufikia mwaka 2011 utakuwa asilimia 5³/₄. Hayo yamesemwa na Bi. Antoinette Monsio Sayeh, ambaye ni Mkurugenzi wa Idara ya Afrika katika Shirika la fedha la kimataifa.

Akizungumza na waandishi mjini hapa, Bi. Sayeh alieleza kuwa Kuzorota kwa uchumi kunategemana sana na hali ya sehemu husika na hii inaonyesha kuwa karibu mbili ya tatu ya nchi za Afrika zimekumbwa na kushuka kwa uchumi na imesababisha serikali zao kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

“Mtikisiko wa kifedha katika nchi unatofautiana kutegemeana na mabara. Kwa nchi zenye kipato cha kati mauzo ya nje yameshuka sana hasa mwanzoni mwa mwaka 2009 kwa sababu ya wanunuzi kuto kuhitaji bidhaa kutoka nchi nyingine. Vilevile hata manunuzi ya mafuta yameshuka sana, na hii imesababisha hata bei ya mafuta kudondoka. Hii inaonyesha kuwa nchi nyingi zenye kipato cha chini zimekuwa na uchumi unakua polepole sana kwa mwaka 2009”. Alieleza Mkurugenzi huyo.

“Kushuka huku kwa uchumi kumesababisha watu kupatashida lakini hii tutaitathimini katika mpango wa maendeleo wa milenia”. Alisema.

Aidha alieleza kuwa itabidi sera za uchumi zirekebishwe ili ziendane na mazingira ya nje. Sera zilizopo zitahitajika kubadilishwa zinahitaji zitengenezwe upya na kuimarisha mifumo ya kifedha ili kujiandaa na lolote baya ambalo linaweza kutokea.

Sera hizi za uchumi sasa zinahitaji kutoka kipindi kifupi na kuwa katika kipindi cha kati chenye malengo ya maendeleo yanayodumu pamoja na uchumi mpana

ulio imara na unaofikirika, labda kama kuna pengo kubwa katika uzalishaji. alisisitiza Sayeh.

Alimalizia kwa kusema kuwa Shirika la fedha la kimataifa lilikuwa bega kwa bega kwa pamoja katika kusaidia kukopesha fedha nchi za Afrika zilizoko katika Jangwa la Sahara kwa mwaka 2009. Zaidi ya dola za kimarekani bilioni 5 zilitengwa na kutolewa. Japokuwa mahitaji yalizidi kuongezeka. Hii inatokana na uhusiano mzuri uliopo kati ya nchi zetu hizi na mashirika hayo ya kifedha.

Imetolewa na Msemaji Mkuu
Wizara ya fedha na uchumi
Washington DC
23/04/2010